**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Nne – Tarehe 22 Disemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2021.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2021.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

36. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwa nia njema, Serikali iliridhia kwa mara ya kwanza tokea kurudishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa kuwepo kwa kura ya mapema iliyopigwa kwa watu maalum siku moja kabla ya uchaguzi mkuu wa Zanzibar 2020. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kuhusu ufanisi na ulazima wake kwa Zanzibar.

(a) Je, nini tathmini ya Serikali kwa kura ya mapema ya tarehe 27 Oktoba, 2021.

(b) Serikali imejipangaje kuboresha chaguzi zinazokuja kufuatia malalamiko yaliyojitokeza.

169. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kituo cha Polisi cha Ng’ambo kinahudumia Wilaya ya Mjini na kinatoa mchango mkubwa katika masuala mbali mbali.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga uzio ili kuimarisha usalama wa kituo hicho.

(b) Ni sababu gani zinazopelekea zoezi la kukiwekea uzio kituo hicho lisifanyike, wakati vituo vyengine vimeshaidhinishwa kwa kuwekwa uzio.

(c) Serikali ina mpango gani wa kuimarisha eneo la nyuma la kituo hicho kwa kujengwa majengo ya kisasa.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

239. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Katika harakati za kupambana na kujipatia kipato, baadhi ya wananchi wamekuwa wakiweka viwanda vya kusagia kokoto karibu sana na maeneo wanaoishi wananchi, jambo ambalo ni hatarishi kwa maisha na afya zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru maisha ya wananchi ili wasidhurike na athari hiyo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

240. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kuna malalamiko ya wananchi ya muda mrefu kuwa katika baadhi ya taasisi za Serikali kuna mtindo wa baadhi ya wakuu wa taasisi hizo kutowapangia kazi watendaji wao wa chini, aidha kwa kuhofia kuwazidi kiutendaji au kwa kulinda maslahi yao na maslahi ya rafiki zao, huku wakijua fika kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyengine zinazohusu maadili ya viongozi wa umma.

Je, Serikali inalitambua suala hilo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

45. MHESHIMIWA SABIHA FILFIL THANI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali kwa kutoa huduma za zimamoto katika maeneo mbali mbali hapa Zanzibar, zinazosaidia kujikinga na majanga ya moto yanayotokea nchini petu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia huduma ya zimamoto maeneo ya visiwani, ukizingatia kuwa magari ya zimamoto hayawezi kuvuka na kufika visiwani huko.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

115. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika kuhakikisha Serikali inadhibiti na hatimae kuongeza makusanyo ya mapato ya nchi, huanzisha mfumo wa makusanyo wa mapato hayo kupitia mtandao. Hata hivyo, katika hali ya kushangaza, hadi hii leo kuna baadhi ya taasisi za Serikali zinatumia risiti za mkono, badala ya kutumia mfumo wa mtandao.

Kwa kuwa matumizi ya risiti za mkono hupoteza mapato, Je Serikali inachukua hatua zipi kuhakikisha taasisi zake zote zinazokusanya mapato zinaachana na mfumo wa risiti hizo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

110. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ni taasisi zipi zinazohusika kuwapatia mikopo nafuu wajasiriamali wetu wadogo wadogo na kwa vigezo vipi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

8. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa mchezo wa kuogelea kwa sasa umepanda chati na kuwa moja ya michezo ya kitaifa na kimataifa na hatimae kuanzishwa mashindano ya ndani na nje ya nchi ambapo nchi mbali mbali hujiandaa kimataifa hususan kwenye mashindano ya OLIMPIC kupitia mchezo huu. Na kwa kuwa Zanzibar ina mazingira mazuri ya kuendeleza na hatimae kuweza kutangaza nchi yetu kupitia mchezo huo.

Je, mashindano ya mchezo huo yameanzishwa hapa Zanzibar.

11. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Baraza la Vijana la Shehia ya Sizini, Wilaya ya Micheweni lilipata bahati ya kupatiwa boti na nyavu zake kwa lengo la kuwapatia ajira vijana hao. Kwa kuwa boti waliyopatiwa ilikuwa ndogo na haikidhi haja iliyokusudiwa.

Je, ni lini Serikali itakamilisha dhamira yake ya kuwapatia vijana hawa boti nyengine kubwa zaidi ili waweze kupambana na umasikini.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

86. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Malengo makubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapatia wananchi wake huduma bora ikiwemo ya maji safi na salama mijini na vijijini.

(a) Je, Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) inafahamu kwamba wananchi wa vijiji vya Bule, Gombe na Kinowe hawapati huduma hiyo.

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zinazopelekea wananchi hao kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

128. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa pale huduma ya kununua umeme kwenye Ezypesa inapokuwa inasumbua na husababisha msongomano mkubwa kwenye vituo vya umeme.

Je, Wizara yako imejipanga vipi kulitatua tatizo hili ili wananchi waepukane na usumbufu huu.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

19. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika malengo yake iliyojiwekea Wizara ina mipango ya kuzijenga barabara za ndani zenye urefu wa kilomita mia mbili (200 km) ili ziweze kupitika muda wote, ingawaje mipango hiyo haijatekelezwa kwa vijiji vyote.

Je, ni lini barabara ya Broo - Bwagamoyo inayotoka kijiji cha Matuuni mpaka kijiji cha Uondwe itajengwa.

87. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali ya awamu ya nane kwa namna inavyoendelea kuwapa matumaini wananchi wake hasa katika kadhia ya ubovu wa miundombinu ya barabara na kuzifanyia maboresho kwa Unguja na Pemba.

Je, ni lini barabara ya Chimba Mambosasa – Konde itajengwa ili kuwaondoshea changamoto za usafiri wananchi wa maeneo hayo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

204. MHESHIMIWA SHADYA MOH'D SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kama tunavyofahamu elimu ndio kila kitu kwa maisha yetu ya sasa. Na ili mtoto aweze kufanya vizuri katika masomo yake ni lazima aanze vizuri kwenye elimu ya awali. Hivi sasa kuna walimu wa TUTU ambao ndio wanaotufinyangia watoto wetu huko chini lakini kumekuwa na usumbufu mkubwa wa suala zima la maslahi yao.

Je, ni lini Serikali kupitia Wizara ya Elimu itafanya jitihada za makusudi kuona kadhiya hii ya muda mrefu kwa walimu hawa inatatuka.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

4. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Uvuvi:

Katika kuweka hali za wananchi sawa pamoja na kufaidika na matunda ya Mapinduzi adhimu ya 1964, marehemu Mzee Abeid Aman Karume, Rais wa awamu ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mashirikiano na Baraza la Mapinduzi aligawa eka tatu tatu za mikarafuu kwa kila Mzanzibari aliyehitaji jambo hilo. Na kwa kuwa ugawaji wa mashamba hayo haukuwa na ubaguzi yaani kila mwananchi alipewa bila ya kujali rangi, kabila au asili yake. Na kwa kuwa hata wale waliokuwa kabla ya Mapinduzi wanamiliki mashamba hayo hawakutengwa, bali na wao walitakiwa wasizidi eka tatu.

Je, ni sababu gani za msingi zilizofanywa na Serikali ya awamu iliyopita kuwanyang'anya mashamba baadhi ya wananchi waliopewa kihalali na Serikali kama ilivyotokea kwenye familia mbali mbali kisiwani Pemba.

82. MHESHIMIWA JUMA ALI KHATIB (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mnamo miaka ya sabiini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilijenga hospitali ya wanyama katika eneo la Mbweni ambayo ilikuwa ikitoa huduma mbali mbali za wanyama. Hata hivyo, kwa kipindi kirefu sasa, jengo hilo la hospitali limekaa bila ya kutoa huduma zozote za wanyama na matumizi yake yamekuwa hayafahamiki.

(a) Je, kwa nini Serikali imeliacha jengo hilo kwa muda mrefu bila ya kulitumia kama ilivyokusudiwa.

(b) Je, jengo hilo kwa hivi sasa linatumika kwa kazi gani.

(c) Je, Wizara ina mpago gani wa kulikarabati au kujenga jengo jengine kubwa zaidi na lenye tija na manufaa mapana zaidi kwa Serikali na wananchi wake kuliko lilivyo hivi sasa.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

31. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Serikali inastahili kupongezwa kwa juhudi zake za kuimarisha afya za wananchi wake sambamba na utunzaji wa mazingira. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba hadi leo nyumba nyingi za baadhi ya vijiji katika jimbo la Pandani (kama vile Kibendera na Mjananza) hazina vyoo wala vyoo vya umma kwa ajili ya wananchi hao.

(a) Je, ni lini Serikali itawajengea wananchi wa Kibendera na Mjananza vyoo vya umma (public toilets) wakati jitihada za kuwasaidia kuwa na vyoo majumbani zikiendelea.

(b) Je, Serikali imefanya tathimini yoyote kugundua idadi ya wananchi wake wasio na vyoo na wanaojisaidia vichakani na misikitini.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali kutatua suala la vyoo kwa wananchi wa Zanzibar.

199. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa mujibu wa matoleo ya Shirika la Afya Duniani (WHO), watoto wachanga wenye umri chini ya miezi sita wanatakiwa kunyonya maziwa ya mama bila kulishwa chakula cha aina nyengine ili kuimarisha afya na ukuaji wa mtoto.

(a) Kwa kuwa Zanzibar inapokea na kufuata maagizo ya WHO, Je, Serikali imechukua hatua gani juu ya agizo hilo.

(b) Kwa kuwa watumishi wengi wa umma wanaendelea kuzaa na kutumia muda mwingi wakiwa kazini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatengea maeneo maalum ya kunyonyesha watoto wao.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

70. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imeahidi kuimarisha viwanda nchini, na kwa kuwa Kiwanda cha Sukari kilichopo Mahonda uzalishaji wake hauridhishi.

(a) Je, ni kiwango gani cha sukari huhitajika Zanzibar kwa mwaka.

(b) Je, katika kiwango hicho kilichotajwa, Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kinatoa tani ngapi ili kukidhi mahitaji hayo.

(c) Je, ni upi mchango wa Kiwanda hiki kwa uchumi wa Zanzibar.

113. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Taasisi ya Viwango Zanzibar (Zanzibar Bureau of Standards (ZBS)) katika kutekeleza majukumu yake, ilizuia mzigo wa 'Oil' na kutoa maamuzi kuwa mzigo huo urejeshwe Dubai ulipotoka. Hata hivyo, wakati wa kuurejesha mzigo huo, ilibainika kuwa, idadi halisi ya mzigo huo imepungua na Taasisi hii imeshindwa kutoa mashirikiano yaliyotarajiwa.

(a) Je, Wizara yako inatoa kauli gani kuhusiana na kadhia hii.

(b) Je, ni hatua gani ambazo Wizara yako imechukuwa au ingelichukua katika kutafuta suluhisho la kadhia hii.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

125. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali inawataka wananchi wake wasingoje ajira za Serikali bali wajiajiri. Wananchi wameitikia wito lakini waanika madagaa wanasumbuliwa sana na watu wanaojiita maajenti wanachukuwa dagaa bila ya kuwalipa.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Kama inalijua, ina mpango gani wa kuwapatia soko la uhakika waanika madagaa hao.

(c) Wananchi wanaowadai maajenti hao kwa muda mrefu sasa Serikali itawasaidiaje.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

144. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Tunaishukuru Serikali kwa kuelimisha wananchi juu ya ujenzi bora na kutumia ramani.

Je, Kwa watu wa hali ya chini wenye kipato kidogo ambao wanajenga chumba kimoja au viwili wakati bei ya ramani keshamaliza chumba chake, kuna utaratibu gani wa kuwasaidi juu ya ramani.

158. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Moja ya malengo maalum ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 ni kuwapatia wananchi wake makaazi bora na katika miaka ya 1970 hadi 2000 Serikali imejenga nyumba nyingi mjini na vijijini. Hata hivyo, muda mrefu umepita tangu kujengwa nyumba hizo na nyingi zimeshachakaa sana.

(a) Kwa kuwa Serikali imebadilisha uongozi wa Shirika la Nyumba na kuleta matumaini mapya ya utendaji bora Je, Serikali ina mpango gani wa kulisaidia Shirika hilo kimtaji ili wajenge nyumba mpya na kuzikarabati zile zilizopo.

(b) Zipo nyumba za vijijini ambazo zimechakaa sana Je, Serikali haioni kwamba muda umefika wa kuziuza nyumba hizo.

**III.** **HOJA ZA SERIKALI:**

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2021.

**IV.** **UCHAGUZI WA VIONGOZI WA MTANDAO WA WABUNGE WA AFRIKA WA KUPAMBANA NA RUSHWA KANDA YA ZANZIBAR.**

**V.** **UCHAGUZI WA VIONGOZI WA JUMUIYA YA WAWAKILISHI KUHUSIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI ZANZIBAR.**

**VI.** **UCHAGUZI WA VIONGOZI WA JUMUIYA YA WAWAKILISHI KUHUSIANA NA IDADI YA WATU NA MAENDELEO ZANZIBAR.**

**Zanzibar,**
**22 Disemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**